

*Shairi lifuatalo liliandikwa na Mshairi Marehemu Hamidu Rajabu Tambwe mwaka 1968 wakati wa vita ya Nigeria na Biafra, mengi yaliyosemwa wakati ule bado yanafanyika katika baadhi ya sehemu Barani Afrika na sehemu mbali mbali duniani.*

### **NIGERIA DHIDI YA BIAFRA.**

- |  |   |
|--|---|
| <p>1. Bismillah Ghafari, kwa jina lako Jalia.<br/>Natunga langu shairi, kuhusu Nigeria.<br/>Kwani ilivyo hatari, siwezi kusimulia.<br/>Mola jalia amani, ifike Nigeria.</p>            | <p>5. Nigeria katili, haachi wake utesi.<br/>Tena kakaa kitili, suluhu yake maasi.<br/>Hili ni jambo dhalili, hasa kwa sisi weusi.<br/>Mola jalia amani, ifike Nigeria.</p>             |
| <p>2. Ndugu wanavyopigana, kwa mabomu na risasi.<br/>Hapana anayepona, wengi wanapita kasi.<br/>Kila iwapo mchana, watu wote wasi wasi.<br/>Mola jalia amani, ifike Nigeria.</p>       | <p>6. Sisi japo ni fukara, tumeuchanga msosi.<br/>Ukufae Biafra, kwa kununua vinyasi.<br/>Ule nao vidoshora, tena bila wasi wasi.<br/>Mola jalia amani, ifike Nigeria.</p>              |
| <p>3. Nigeria hakika, ni nchi yenye wakwasi.<br/>Lakini yasikinika, kazi ya hao waasi.<br/>Fedha zote watumika, kununulia risasi.<br/>Mola jalia amani, ifike Nigeria.</p>             | <p>7. Na mwisho wa yote haya, tunamuomba Qudusi.<br/>Avushe mambo mabaya, yenye hizi kwetu sisi.<br/>Tuwe wenye kutulia, tukae bila tatasi.<br/>Mola jalia amani, ifike Nigeria.</p>    |
| <p>4. Biafra wamtwanga, kana kwamba si mweusi.<br/>Mwisho anakosa unga, na kukonda kama mbesi.<br/>Haya mambo ya kijinga, ni aibu kwetu sisi.<br/>Mola jalia amani, ifike Nigeria.</p> | <p>8. Ndimi mimi mwana Sangu, Sheikh Tambwe mahsusi.<br/>Hizi beti nane zangu, zije kwenu mafarisi.<br/>Kaeni bila mizungu, mzidi kupiga kasi.<br/>Mola jalia amani, ifike Nigeria.</p> |

*Hamidu R. Tambwe  
Mbeya-Tanzania  
Septemba, 1968*